

## JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

### BUNGE LA TANZANIA

Tele: +255 026 2322761-5  
Fax No. +255 026 2324218  
E-mail: [cna@bunge.go.tz](mailto:cna@bunge.go.tz)

Ofisi ya Bunge  
S.L.P. 941  
**DODOMA.**



### TAARIFA KWA UMMA

Kamati za Kudumu za Bunge tatu (3) zimepanga kufanya vikao vyatupokea na kusikiliza maoni ya Wadau kuhusu Miswada Mitano (5) ya Sheria kama ifuatavyo:-

- Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji itapokea na kusikiliza maoni ya wadau kuhusu **Muswada wa Sheria ya Huduma za Maji na Usafi wa mazingira wa Mwaka 2018 (The Water Supply and Sanitation Bill, 2018)**. Kikao hicho kitafanyika tarehe **16 Januari, 2019** katika ukumbi Na.43 Jengo jipya la Utawala, Bungeni Jijini Dodoma kuanzia **saa 3:00 Asubuhi**.
- Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu itapokea na kusikiliza maoni ya wadau kuhusu **Muswada wa Sheria ya Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania wa Mwaka 2018 (The Tanzania Meteorological Authority Bill, 2018)** tarehe **17 Januari 2019** na **Muswada wa Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri wa Ardhini wa Mwaka 2018 (The Land Transport Regulatory Bill, 2018)** tarehe **18 Januari, 2019**. Vikao hivyo vitafanyika katika ukumbi Na. 38 Jengo jipya la Utawala, Bungeni Jijini Dodoma kuanzia **saa 3:00 Asubuhi**.

- Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria itapokea na kusikiliza Maoni ya Wadau kuhusu **Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Vyama vya Siasa wa Mwaka 2018 (The Political Parties (Amendments) Bill, 2018)** na **Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 4) wa Mwaka 2018 (The written Laws [Miscellaneous Amendments](No. 4) Bill, 2018)** tarehe **17** na **18 Januari, 2019** katika ukumbi Na. 9 Jengo Kuu la Utawala. Aidha tarehe **19** na **20 Januari, 2019** Kamati itapokea na kusikiliza maoni ya **wawakilishi kutoka kila Chama cha Siasa kilichosajiliwa nchini** kuhusu **Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Vyama vya Siasa wa Mwaka 2018 ( The Political Parties (Amendments) Bill, 2018)**

Kamati zinawaalika wadau kufika na kuwasilisha maoni yao kwa lengo la kusaidia katika uchambuzi wa miswada hiyo ambayo inapatikana katika Tovuti ya Bunge [www.parliament.go.tz](http://www.parliament.go.tz). Aidha maoni ya wadau yanaweza kuwasilishwa kwa njia ya Posta au Baruapepe kwa anuani ifuatayo:-

Katibu wa Bunge,  
Ofisi ya Bunge,  
S.L.P 941,  
**DODOMA.**  
Baruapepe: [cna@bunge.go.tz](mailto:cna@bunge.go.tz)

**Imetolewa na:-**

Kitengo cha Habari, Elimu kwa Umma na Mawasiliano,  
Ofisi ya Bunge,  
S.L.P 941,  
**DODOMA.**